TANGAZO LA SERIKALI NA. 525 la tarehe 28/6/2024

SHERIA YA MISITU
(SURA YA 323)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 29(1))*

AMRI YA KUTANGAZA MABADILIKO YA MPAKA WA MSITU WA HIFADHI UYUI KIGWA RUBUGA YA MWAKA 2024

Jina

**1**. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutangaza Mabadiliko ya Mpaka wa Msitu wa Hifadhi Uyui Kigwa Rubuga ya Mwaka 2024.

Tangazo

Ts. Na. 509 la 1958

**2**. Eneo la ardhi ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Tangazo la Msitu wa Hifadhi Uyui Kigwa Rubuga linafanyiwa mabadiliko kusomeka na kuonekana kama lilivyochorwa katika Ramani iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA UYUI


MSITU WA HIFADHI UYUI KIGWA RUBUGA

*Makadirio ya eneo:* Hekta 98489.12 au Kilometa za Mraba 984.89

Unakopatikana na Mipaka

Eneo lote la hifadhi awali chini ya Msitu wa Hifadhi wa Uyui Kigwa Rubuga linalopatikana Wilaya ya Uyui, Mkoa wa Tabora kama lilivyochorwa katika Mpango wa Idara ya Upimaji Jb 2773 ya mwaka 2018 (Skeli 1:50,000) uliohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Upimaji na Ramani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na lenye mipaka ifuatayo:

*Tangazo la Serikali Na. 525 (Linaendelea)*




Dodoma,
24 Mei, 2024

ANGELLAH JASMINE KAIRUKI,
*Waziri wa Maliasili na Utalii*